

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Anuani ya Simu "TAMISEMI"
DODOMA
Simu Na: +255 26 2321607
Nukushi: +255 26 2322116
Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz



**Mji wa Serikali – Mtumba,
Mtaa wa TAMISEMI,
S.L.P. 1923,
41185 DODOMA.**

TANGAZO LA KUITWA KAZINI

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inawataarifu waombaji wote walioomba nafasi ya ajira za Ualimu na Kada za Afya kuanzia tarehe **20/04/2022** hadi **08/05/2022** kuwa zoezi la uchambuzi wa maombi yaliyopokelewa limekamilika. Aidha, waombaji wa nafasi za ajira ya Ualimu na Kada za Afya waliokidhi vigezo wamepangiwa kazi katika Hospitali, Vituo vya Afya, Zahanati, Shule za Msingi na Sekondari katika Halmashauri mbalimbali nchini.

Waombaji waliopata ajira na kupangiwa vituo vya kazi wanatakiwa kuzingatia maelekezo yafuatayo:-

1. Kuripoti katika vituo vya kazi walivyopangiwa katika Halmashauri mbalimbali nchini ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili. Waombaji watakaoshindwa kuripoti kwenye vituo vya kazi walivyopangiwa ndani ya siku 14, nafasi zao zitajazwa na waombaji wengine wenye sifa haraka iwezekanavyo.
2. Kuwasilisha kwa waajiri wao (Wakurugenzi wa Halmashauri walizopangiwa) vyeti halisi (**Original Certificates**) kwa ajili ya kuhakikiwa na waajiri kabla ya kupewa barua za ajira. Vyeti hivyo ni kama ifuatavyo:
 - i. Cheti cha Kuzaliwa;
 - ii. Kitambulisho cha Taifa au Namba ya Utambulisho ya NIDA;
 - iii. Cheti cha Kidato cha Nne na au Sita;
 - iv. Cheti cha kuhitimu Shahada (Degree), Stashahada (Diploma) na Astashahada (Certificates) katika Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali;
 - v. Cheti cha Usajili kutoka Mabaraza ya Kitaalamu katika Sekta ya Afya kwa kada husika; na
 - vi. Uthibitisho wa kumaliza Mafunzo kwa Vitendo (*Internship*) kwa kada husika.
3. Kwa waombaji waliosoma nje ya nchi na wamepata ajira kwa kada husika wanatakiwa kuwasilisha vyeti vya ithibati (Accreditation Certificates) kutoka NECTA, NACTEVET au TCU.
4. Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wahakikishe wanapokea vyeti na kuviwasilisha Baraza la Mitihani kwa ajili ya uhakiki. Kwa wale ambao watakuwa na vyeti vya kughushi hatua kali zichukuliwe juu yao.

Orodha ya waombaji waliopata ajira na vituo vyao vya kazi walivyopangiwa katika Halmashauri mbalimbali nchini inapatikana kupitia tovuti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI: www.tamisemi.go.tz.

Limetolewa na:-

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais - TAMISEMI

26 Juni, 2022